**Maswali na Majibu**

*1.* Mbona Mungu alimjaribu Ibrahimu?
*Alitaka kujua kama Ibrahimu anampenda kuliko vyo vyote.*

2. Mungu aliambia Ibrahimu afanye nini?
*Alimwambia achukue Isaka mpaka kwa nchi ya Moria na amutoe kama dhabihu*.

*3.* Ibrahimu aliamini kwamba Mungu atafanya nini kwa kutimiza ahadi yake?
*Ingewezekana Mungu amfufue Isaka kutoka kwa wafu.*

4. Nini ilifanyika wakati Ibrahimu alitaka kumua Isaka?
*Malaika alimwambia amwachilie Isaka. Badala yake alitoa kondoo mume*.

*5.* Hadithi hii inalinga Yesu namna gani?
*Mwana wa pekee, siku 3 kwa wafu au kifo kiliadhiriwa, Mlima wa Moria, beba kuni/msalaba, kondoo Mume/ mwana kondoo, hai baada ya siku 3*

6. Mbona Ibrahimu hakutaka Isaka aoe mwanamke Mkanaani?
*Kwa sababu waliabudu sanamu. Alitaka mke anayependa Mungu*.

*7.* Eliezeri alipataje mke mwenye Mungu alimchagulia Isaka?
*Aliomba kwamba yule mwanamke atampa yeye na ngamia zake maji ya kunywa.*

8. Tufanye nini kwa maisha yetu kabla tuamue kufanya jambo? *Tuombe Mungu*.

9. Mungu alichagua mwanamke yupi? Alikuwa wa jamii ipi?
*Rebeka. Alikuwa mjukuu wa nduguye Ibrahimu*.

*10.* Mbona Isaka na Rebeka walitakiwa wawe na mwana?
*Kutimiza ahadi zenye Mungu alikuwa ameahidia Ibrahimu.*

## Mistari ya kukariri

Mwanzo 22:16 – 17 Yohana 3:16

## Mazungumzo

Zungumza juu ya mke gani mwenye Ibrahimu alitaka awe wa mwanawe Isaka. Ukitaka mwenziko wa ndoa unatakiwa uchunguze nini?

## Kuandika

Andika na ulinganishe hadithi ya Ibrahimu kwenda kumtoa Isaka kama dhabihu na vile inalenga kwa Yesu naye kama dhabihu. Inaendaje sambamba?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 8 Isaka

**SOMA Mwanzo 22:1 – 19 na Mwanzo 24**


**SOMO**

Isaka alikuwa mwana wa Ibrahimu. Alipokuwa akikua alijifunza kupenda na kumtii Mungu. Isaka alijua kwamba ahadi za ajabu za Mungu zitapitishwa mpaka kwake. Alijua ataishi kwa nchi ya Kanaani yenye Mungu aliahidi baba yake, Ibrahimu. Wazao wake watakuwa taifa kubwa na watakaa kwa hiyo nchi. Mmoja wa uzao wake ataleta furaha kwa mataifa yote.

Isaka alikua na akawa kijana mkubwa. Ibrahimu alimpenda sana kwa kuwa alikuwa mtoto wa kipekee. Mungu alitumia Isaka kujaribu imani ya Ibrahimu kuona kama anampenda yeye Mungu kuliko vyote. Siku moja Mungu alimwambia Ibrahimu kuchukua Isaka na waende kwa nchi ya Moria na amtoe Isaka kama dhabihu ya kuteketeza.

Ibrahimu alitii Mungu. Alijua kwamba Isaka ni mwana aliyeahidiwa na Mungu. Alijua kwamba inabidi awe na mwana ili ahadi za Mungu zikamilike. Lakini Ibrahimu aliamini kwamba Mungu atatimiza ahadi zake. Ibrahimu aliamini kwamba, ikiwezekana, Mungu atafufua Isaka kutoka kwa wafu.

Ibrahimu aliamka kesho yake mapema. Alichukua Isaka, watumishi wawili, kuni, moto na kisu. Walisafiri kwa siku tatu ili wafike kwa nchi ya Moria. Walipofika kule, Ibrahimu aliambia watumishi wakae pale, na Isaka na yeye waende juu mlimani kusujudia Mungu na warudi wote wawili. Ibrahimu aliamini kwamba Mungu atafufua Isaka kutoka kwa wafu.



Isaka alibeba kuni. Aliuliza baba yake, “Tuko na kuni na moto lakini wapi mwana kondoo kama sadaka ya kuteketezwa?” Ibrahimu alijibu, “Mwanangu, Mungu ataleta huyo mwana kondoo wa sadaka.”

Walipofika juu mlimani, Ibrahimu alijenga madhabahu. Aliweka kuni na Isaka juu ya hiyo madhabahu. Ibrahimu alichukua kisu na akataka kuua Isaka.

Halafu alisikia malaika akiita jina lake. Malaika aliita na kusema, "Usimuumize kijana! Sasa najua kwamba unampenda Mungu kwa sababu umeamua kuua mwanao wa pekee. Nitakubariki." Ibrahimu alifarijika. Alimwaajilia Isaka akaenda. Ibrahimu aliangalia huku na kule na akaona mwana kondoo mume ameshikwa kwenye kichaka. Ibrahimu alimtoa kama sadaka kwa madhabahu. Mungu alifurahia Ibrahimu na kumpenda sana hata akarudia hizo ahadi kwa Ibrahimu.


Undani wa hadithi hii inalingana na kuenda sambamba na dhabihu ya Yesu.

| | |
|---|---|
| Isaka alikuwa **mwana wa pekee** wa Ibra-himu | Yesu alikuwa **mwana wa pekee** wa Mungu |
| Kwa **siku 3** Ibrahimu alipanga kuua Isaka | Kwa **siku 3** Yesu alikwa maiti kwa kaburi |
| Ibrahimu alienda kutoa Isaka kama dhabihu kwa **Mlima wa Moria** | Yesu aliuawa kwa **Mlima wa Moria** nje ya Yerusalemu |
| Isaka alibeba **kuni** | Yesu alibeba **msalaba** |
| Ibrahimu alitolea Mungu **mwana kondoo wa kiume** | Yesu alikuwa **mwana kondoo** wa Mungu aliyeuawa |
| Baada ya safari ya siku 3 kwenda kuawa Isaka, alirudi nyumbani **akiwa hai** | Baada ya siku 3 kaburini, Yesu alikuwa **hai tena** |

Ibrahimu alijua ni jambo la maana mrithi wa hizo ahadi aoe mwanamke anayempenda Mungu. Wakanaani waliishi kwa nchi yenye Ibrahimu aliishi. Wakanaani waliabudu sanamu. Kwa hivyo Ibrahimu hakutaka Isaka aoe mke wa Kanaani.

Kwa hivyo Ibrahimu aliita mtumishi wake, Eliezari akamwambia aende Harani na amchagulie Isaka mke kutoka kule. Ibrahimu alijua kwamba jamii yake waliishi kule na waliabudu Mungu. Alimwambia kwamba Mungu atamsaidia achagulie Isaka mke mzuri. Eliezari aliahidi kufanya hivyo. Alichugulia yule mke zawadi na akaanza safari mrefu ya kwenda Harani.

Mapema ya jioni moja Eliezari alifika Harani. Aliona kisima nje ya ukuta wa mji. Alijua jioni kama hiyo wanawake vijana wa mji watakuja kuteka maji. Eliezari aliomba Mungu amsaidie apate mke mzuri. Eliezari aliomba hivi, "Mwanamke atakaye kubali kuchotea ngamia zangu kinywaji yeye ndiye utakuwa umemchagua awe mke wa Isaka."



Mwanamke kijani alikuja kwa kisima. Eliezari alimwomba maji anywe. Yule mwanamke alimpa na hata akachotea ngamia zikanywa. Eliezari alimuuliza jina lake. Jina lake lilikuwa Rebeka. Alikuwa ni binti wa Nahori nduguye Ibrahimu. Eliezari alijua kwamba Mungu alikuwa amemsaidia. Eliezari alimpa Rebeka pete na vipuli vya dhahabu. Eliezari alimuuliza kama angeshinda kwao usiku kuja.

Eliezari aliendа na akakutana na familia ya Rebeka. Eliezari aliwambia sababu yake ya kukuja Harani. Baba na nduguye Rebeka walikubali Rebeka aoleke kwa Isaka ikiwa mwenyewe atataka.

Asubuhi iliyofuata, waliuliza Rebeka kama angeenda na Eliezari. Alijibu, "Nitaenda." Eliezari na Rebeka walianza safari ya kwenda kwa nchi ya Israeli yenye Ibrahimu aliishi.

Jioni moja baada ya kusafiri kwa muda mrefu, Rebeka aliona mwanamume anatembea shambani. Huyo mwanamume aliangalia juu na akaona ngamia zinakuja, halafu akaenda kukutana nao. Rebeka alitaka kujua yeye ni nani. Eliezari alimwambia kwamba yeye ni Isaka. Rebeka alijifunika uso kwa utaji.

Rebeka alikaa kwa hema la Sara mpaka alipooleka kwa Isaka. Isaka alimpenda Rebeka. Alikuwa mwanamke mtawa na mwenye imani. Mungu alikuwa amemchagua awe mke wa Isaka.

Mungu alimuahidi Isaka kwamba wazao wake watakuwa wengi. Kwa hivyo Isaka alitakiwa awe na mwana ili atimize hizi ahadi. Baada ya miaka mingi, Isaka na Rebeka walipata wana wawili, Yakobo na Esau.

Ibrahimu alitaka Isaka awe na mke mzuri. Alitaka awe na mke aliye na imini kwa Mungu, kwa sababu angesaidia Isaka awe na imani. Ingekuwa vigumu Isaka kuabudu Mungu kama angempata mke aliyetaka kuabudu sanamu. Mke aliye na imani kwa Mungu anaweza kusaidia mumewe. Ibrahimu alituonyesha mfano mzuri kwa kumtafutia Isaka mke mcha Mungu. Tunapotafuta mke au mume ni vyema kutafuta yule aliye na imini kwa Mungu; mwenzio atakayekusaidia kumpenda Mungu.